# Uchambuzi Wa Fani Katika Riwaya Ya Mzingile

A commentary on Kiu.
On the role and importance of oral literature in the development of written literature.
A commentary on some Swahili novels from Zanzibar.
Diwani hii imegawanywa kwenye sehemu kuu tatu, ambazo zimepewa jina la milango ya falsafa, na kila mlango unajishughulisha na dhamira zinazofanana chini ya maudhui moja kuu. Mlango wa kwanza umeitwa Mlango wa Falsafa za Siasa (Uk. 1), ambapo tungo zilizomo ndani yake zinajikita kwenye dhamira zinazoakisi mahusiano baina ya watawala na watawaliwa, harakati za kiraia za kudai haki na hata suto kwa watawala juu ya namna wanavyoyatumia madaraka yao. Ni ndani ya mlango huu munamojitokeza utungo uliobeba jina la diwani hii, Mfalme Ana Pembe (Uk. 4).Sehemu ya pili inaitwa Mlango wa Falsafa za Maisha (Uk. 35). Tungo zilizomo humu zinajikita kwenye kuzungumzia maisha katika ngazi na mbeya mbalimbali - tangu mahusiano ya kifamilia hadi urafiki na hata maongezi ya mtu na nafsi yake katika nyakati za kuyakabili maisha, ama iwe kwenye nyakati za furaha au za majonzi. Na Mlango wa Falsafa za Mapenzi (Uk. 67) ndiyo sehemu ya tatu na ya mwisho ya diwani hii, ambayo inaliangalia suala la mahusiano ya kimapenzi katika hali na sura zake kadhaa - kupenda, kupendwa, kukataa, kukataliwa, raha na karaha zake.Lengo la kuwekwa muundo huu ni kumsaidia msomaji kuogelea haraka kwenye bahari ambayo

angeliipendelea au kwenda kwenye maji hayo pindi akitaka, bila kulazimika kupiga mbizi huku na kule na kujikuta amerowana kabla ya kupata akitakacho. Hii haimaanishi kuwa kuna sehemu iliyopangiwa iepukwe wakati wa kuisoma diwani hii. La hasha! Kila mshororo, kila ubeti, kila utungo, na hata kila neno, linastahiki kusomwa kwa uzito na stahiki yake kwenye diwani nzima.Kisha, kila mlango kati ya milango hii mitatu, unafunguliwa kwa hadithi ya paukwa-pakawa, ambayo imeteuliwa kutoka hadithi nyingi za aina hiyo, ikiakisi maudhui ya jumla ya mlango mzima. Si lazima kuwa hadithi hiyo igusane moja kwa moja na kila utungo uliomo kwenye mlango, lakini kuna kiwango cha mshikamano baina ya tanzu hizi mbili kongwe za fasihi - nganu za kale na ushairi.Kitu chengine kwenye mjengeko wa diwani hii, ni kuwa kila utungo umewekewa maswali matatu, ambapo angalau mojawapo linahusu fani ya sanaa hii kongwe na adhimu. Lengo ni kuwasaidia wale ambao wanasoma diwani hii sio tu kwa kustaaladhi kwa lugha na mawazo yaliyomo ndani yake, bali pia kwa kujifunza uandishi, uchambuzi na uhakiki wa ushairi. Wanafunzi, walimu na watafiti wa taaluma za fasihi - makhsusi wanaoogelea kwenye bahari za tungo - wanaalikwa kuyatumia maswali hayo kama muongozo wa kuifahamu kazi hii. Hata hivyo, nalo halimaanishi kuwa milango ya kubuni maswali na kuibua mijadala mingine juu ya diwani hii imefungwa! Hapana, ruhusa inatolewa kwa watajwa hapo juu kuyatanua, kuyaongeza, kuyapungunza, kuyabadilisha na hata kuyaondoa kabisa maswali yaliyopo kwenye kila mwisho wa utungo, ikiwa kufanya hivyo kutawasaidia kufahamu zaidi kazi hii.Vile vile, na kwa

madhumuni hayo hayo ya kuwasaidia wasomaji, kila mwanzoni mwa utungo, baadhi ya misamiati migumu imeorodheshwa na kuandikiwa tarjumi yake. Mengi ya maneno haya ni ya Kipemba, lugha ambayo ndiyo aliyozaliwa na kukulia nayo mtungaji wa diwani hii. Kwa kuwa Kipemba ni lahaja inayojitegemea kwenye misamiati na hata miundo ya sentensi zake, baadhi ya wakati inamuwia shida kwa mzungumzaji wa kile kiitwacho Kiswahili Sanifu pekee kufahamu maana ya maneno au vifungu vya maneno. Inatazamiwa kuwa uchambuzi huu wa awali wa misamiati, utamsaidia msomaji wa aina hiyo.Mohammed Khelef GhassaniJanuari 2018Bonn - Ujerumani

On the fundamentals of oral literature.

On literary criticism of oral literature giving types and descriptions of each genre of oral literature.

Theory of literary criticism.

Johari ya kiswahilikidato cha tatuEast African PublishersMwongozo wa WalenisiEast African PublishersMsururu wa PTE KiswahiliEast African PublishersJohari ya Kiswahili 3East African PublishersRiwaya ya KiswahiliUhakiki na uchambuzi wa riwaya na ushairi

A guide to Swahili literature with questions and answers for secondary and tertiary institutions.

On the theme of faith and ideology in Robert Shaaban's works.

On the Swahili language in the 21st century.

Short stories.

Miaka Hamsini ya Kiswahili Nchini Kenya ni mkusanyiko wa makala yaliyowasilishwa katika kongamano la kimataifa la Kiswahili lililoandaliwa na Chama cha Kiswahili cha

Taifa (CHAKITA) mwaka 2013, na likafanyika katika Chuo Kikuu cha Kikatoliki cha Afrika Mashariki (CUEA). Makala chache zimetokana na kongamano la mwaka 2012 lililofanyika katika Chuo Kikuu cha Kenyatta. Kitabu hiki kinadhihirisha umuhimu wa lugha ya Kiswahili katika nyanja mbalimbali za jamii. Kwa hiyo, utapata humu ndani makala yanayoangazia ufundishaji wa lugha ya Kiswahili; Kiswahili kama nyenzo ya maendeleo ya uchumi wa taifa; mchango wa Kiswahili katika kuleta uwiano na utangamano wa kitaifa; utafiti wa Kiswahili katika lugha na fasihi; Kiswahili na ujenzi wa taswira ya mwanamke; fasihi ya watoto katika Kiswahili; na athari za Sheng kwa Kiswahili. Kwa ufupi makala yaliyomo humu yanashadidia maendeleo ya Kiswahili katika miaka hamsini iliyopita nchini Kenya. Hiki ni kitabu muhimu sana kwa wanafunzi na walimu wa Kiswahili. Pia ni kitabu kitakachomnufaisha yeyote anayependa Kiswahili na anayetambua mchango wake katika jamii. Fifty Years of Kiswahili in Kenya is a collection of articles that were presented at an international Kiswahili conference organized by the National Kiswahili Association (CHAKITA) Kenya in 2013, which was held at the Catholic University of Eastern Africa (CUEA). A few articles are however from a similar conference held in 2012 at Kenyatta University. The book exemplifies the importance of the Kiswahili language in various sectors of society. Therefore, within this book you will find articles that focus on the teaching of the Kiswahili language; Kiswahili as a tool for national economic development; the contribution of Kiswahili to national cohesion and integration; Kiswahili research in language and literature; Kiswahili and

portrayal of women; children’s literature in Kiswahili; and how Sheng affects Kiswahili. In short, the articles herein are a testimony of how Kiswahili has developed in the last fifty years in Kenya. This is a very important book for Kiswahili students and teachers. It is also an invaluable text for Kiswahili enthusiasts and all those who recognize its contribution to society.

On literary criticism of prose and poetry, based on five Swahili literary works.

Copyright: 1d8c542b2cc25c546cc4209e1433bfdb